Matumizi ya Lugha Hasi Yanavyoathiri Malezi ya Watoto, Ujifunzaji na Mustakabali wa Maisha Yao

Rose Sekile
Idara ya Lugha, Isimu na Fasihi
Chuo Kikuu cha Kikatoliki Mbeya
Barua pepe: rosesekile80@gmail.com

Na

Sebastian Nyerere Mbwillow
Idara ya Lugha, Isimu na Fasihi
Chuo Kikuu cha Kikatoliki Mbeya
Barua pepe: nyererembwillow@gmail.com

Ikisiri

Makala haya yanahusu matumizi ya lugha katika malezi yanavyoathiri ujifunzaji na mustakabali wa maisha yao. Kimsingi, makala yanalenga kujadili matumizi ya lugha hasi katika malezi na tendo zima la ujifunzaji. Aidha, makala yanalenga kuielekeza jamii jinsi lugha ilivyo na mchango mkubwa wa kuweza kujenga utu na kumuandaa mtu bora, au mbaya, kuzindua fikra za wanajamii ili wawe na mtazamo chanya kuhusu matumizi lugha wakati wa kulea watoto. Data zilizofanikisha makala haya zilitokana na utafiti wa uwandani kwa kiasi kikubwa na kimaktaba kwa kiasi kidogo. Data za msingi zilipatikana katika jamii. Data hizi zilipatikana kwa wazazi, walimu na wanafunzi walioko shule za msingi, sekondari, na vyuo. Mbinu ya usomaji makini na upembuzi yakinifu zilitumika kupata data za msingi. Nadharia iliyoongoza uchanganuzi wa data ni Nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano ya Dell Hymes (1974). Makala haya yanaonesha kuwa lugha hasi zimekuwa zikizungumzwa katika miktadha mbalimbali kama nyumbani, kwenye elimu, na katika jamii. Fauka ya hayo, matumizi ya lugha hasi katika miktadha tajwa huacha athari hasi kwa watoto hasa kisaikolojia. Makala haya yanahitimisha kwa kuitaka jamii iwe na uelewa mpana kuhusu matumizi ya lugha wakati wa malezi, kwa sababu lugha inayotumika inaweza kuwaathiri watoto. Watoto ni sehemu kubwa ya jamii, na ndiyo tegemeo la uendelevu wa taifa lolote, hivyo hatuna budi kuwalea vizuri na kuwaendeleza ili waweze kutimiza ndoto zao.

Maneno Muhimu: *Lugha, Malezi*, *Ujifunzaji*, *Mustakabali*

1.0 Utangulizi

Matumizi ya lugha ni namna ya kutumia lugha kulingana na mila, desturi na taratibu zilizopo katika jamii husika. Ni vile ambavyo mzungumzaji anatumia lugha yake ili kuhusiana na msikilizaji. Massamba (2009:45) anafafanua kuwa lugha ni mfumo wa sauti nasibu ambazo

zimebuniwa na jamii kwa madhumuni ya mawasiliano kati yao. Hivyo basi, lugha ina kazi zaidi ya kutimiza jukumu lake mujarabu la mawasiliano.

Tangu tumboni mwa mzazi, mtoto huanza kuwasiliana na mama yake kwa kusikia sauti ya mzazi. Mtoto anapozaliwa huanza mazungumzo kupitia lugha ya mzazi, ambayo inamjengea msingi wa msamiati. Ni wajibu wa mzazi kutumia lugha chanya itakayomuwezesha mtoto kutenda na kuhusiana na watu kikamilifu. Verial (2018) anaeleza kwamba tangu kuzaliwa, mahusiano ya wazazi hujenga mazingira ya kifamilia ambamo watoto hulelewa. Mahusiano haya huweza kuleta athari za kudumu kwa watoto.

Pamoja na kuwasiliana, lugha hujenga tabia ya mtu; hii hutegemea sana watu wanaomzunguka mtu huyo wanazungumza nini, ambacho kwacho yeye kama mpokeaji lugha hukipata. BAKITA (2022) wanadadavua dhana ya athari kuwa ina maana tatu: kwanza, ni jeraha, kidonda, au kovu linalobakia baada ya kiumbe kuumia au kujeruhiwa; pili, doa, alama au kutu ambayo hukipata kitu kinapokuwa kwenye mazingira yasiyofaa; na tatu, matokeo mazuri au mabaya yampatayo mtu au kitu baada ya kupitia hatua fulani. Udadavuzi huu wa tatu ndiyo hasa tumetumia katika makala haya kuonesha taathira za matumizi ya lugha (hasa mabaya) kwa mtoto. Hii ni kwa sababu tunaamini lugha husaidia sana katika kumjenga mtu tangu utotoni. Walezi na walimu, kwa kujua au kutojua, huathiri wanafunzi kwa lugha wazitumiazo mbele ya hao watoto/wanafunzi.

Malezi ni mchakato endelevu wa maandalizi ya mtoto utakaomwezesha kukua, kukubalika na kushiriki katika shughuli za jamii. Mchakato huu unahusisha matumizi ya lugha kwa sehemu kubwa. Ili kumuwezesha mtoto kukua mathalani kiakili, ili kimo na weledi wa mambo vikue sambamba, wazazi, walimu na jamii kwa ujumla hawana budi kuwekeza muda wao kumuandaa mtoto. Verial (2018) anasema kuwa chembechembe za mwili anazozaliwa nazo mtoto na mazingira anamoishi huathiri tabia zake. Verial (keshatajwa) anasisitiza kuwa kila kinachotokea katika jamii huwafunza watoto namna ya kuishi ulimwenguni. Kwa mfano, semi mbalimbali wanazokumbana nazo watoto kutoka kwa wazazi, walimu na jamii zinawafunza namna ya kuishi katika jamii.

Mochiwa (2007) katika makala yake ya ‘Utoto hadi Ungumbaru: Matatizo ya Elimu’, anatoa maelezo kuntu kuhusu suala la malezi huku akihusisha na ukuaji wa lugha. Mochiwa

(keshatajwa) anasema malezi ni kipindi kinachoanzia pale ambapo mwanadamu anapambana na mazingira. Yaani, malezi huanza tangu mtoto anapozaliwa. Wakati huo, wazazi au walezi wana wajibu wa kuhakikisha mtoto analelewa na kukua vema. Kitendo hicho cha kumwongoza mtoto kutoka kutojifahamu hadi kujifahamu na kuwa mtu mwenye kujichunga na kujiongoza ndicho huitwa kipindi cha ulezi. Ingawa hapa anatajwa mzazi au mlezi kuwa ndiyo mwenye jukumu la ulezi, hata hivyo, bado kuna watu wengine kama vile walimu, ndugu, jamaa na jamii kwa ujumla wenye jukumu la ulezi wa mtoto. Ndiyo maana katika makala yetu tunaangazia jinsi walezi hawa wanavyotumia lugha na athari ya lugha hiyo katika makuzi ya mtoto.

2.0 Nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano

Kwa mujibu wa Hudson (1980) na Fasold (1990), Nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano iliasisiwa na Dell Hymes (1964). Ethnografia hasa mawasiliano ni uchanganuzi wa lugha na jukumu lake katika jamii husika. Nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano ni mwegemeo jumuishi wa utafiti unaotumia misingi ya kiethinografia kuchanganua mawasiliano yoyote yale, pamoja na kuchunguza mazingira yanamotokea. Nadharia hii hufanya hivi ili kutambua mazingira halisi ya kitamaduni na kimuktadha ambamo mawasiliano hutokea (Kyeu, 2021). Kyeu (keshatajwa) anafafanua upekee wa nadharia hii kuwa inaupekee wake katika jinsi inavyochanganua viambajengo vya mawasiliano kama vile, washiriki kwenye mawasiliano, mazingira, muktadha na njia wanazotumia washiriki ili kufanikisha mawasiliano.

Nadharia hii ni mtazamo wa isimu jamii unaojikita katika vipengele vikuu vitatu: muktadha, utamaduni, na mazingira mbalimbali katika jamii ili kuoanisha lugha na matumizi yake. Mtazamo huu huchunguza jinsi tukio fulani katika jamii linavyoibua matumizi maalum ya lugha ili kufanikisha malengo yaliyokusudiwa. Aidha, huchunguza jinsi wahusika wa lugha wanavyotumia lugha hiyo kwa kutekeleza majukumu yao ikiwa ni pamoja na kushauri, kuonya, kutia moyo, kukashifu, kubembeleza, kuliwaza, kukejeli tabia mbaya, kueleza hisi mbalimbali, kuhifadhi utamaduni, kuwasiliana, na kuburudisha. Wafuasi wa nadharia hii wanaamini kuwa matumizi ya lugha hayawezi kutenganishwa na utamaduni wa jamii; yaani mila, desturi na itikadi za jamii hiyo. Nadharia hii ina misingi yake katika jamii lugha, na inapotumiwa huchunguza jinsi mawasiliano yanayotumia lugha huendeshwa.

Kwa mujibu wa Hymes (1962, 1964, 1974), vipengele vya mada, ujumbe, lugha, wahusika na mazingira ndiyo mihimili ya nadharia hii. Crystal (1977) anasema kuwa, mada inayozungumzwa ni kipengele muhimu katika mawasiliano. Maudhui ya ujumbe unaowasilishwa yanakuwa nguzo muhimu katika kuteua maneno mwafaka katika mawasiliano. Kwa mujibu wa Crystal (keshatajwa), kinachovutia katika kuibua maana katika sanaa ni muktadha wa maongezi. Muktadha huchukua wajibu mkuu katika kubainisha jinsi maneno mahsusi yanavyobainishwa katika tukio hilo. Gregory na Carroll (1978) wanasema kwamba, maneno huibua maana kulingana na muktadha, hivyo basi, muktadha ni muhimu katika kutafsiri matukio na kuwasilisha ujumbe kwa wanajamii. Aidha, muktadha wa kijamii ambapo tukio hufanyika huchangia kwa sehemu kubwa uteuzi wa aina ya lugha ifaayo kutumiwa kuwasilisha ujumbe miongoni mwa wanajamii. Matumizi ya muktadha kama kitengo kikuu cha nadharia ya mawasiliano katika utafiti huu yaliwezesha kubainisha miktadha tofauti ya matumizi ya lugha ambayo ndiyo inajadiliwa katika utafiti huu, ikiwamo muktadha wa nyumbani, muktadha wa kielimu, na muktadha wa kijamii. Mihimili hii ilitumika katika utafiti huu kuchunguza na kufafanua watumiaji wa lugha na namna wanavyoitumia lugha katika mawasiliano ili kufikisha ujumbe uliokusudiwa kwa walengwa.

3.0 Mbinu za Utafiti

Katika sehemu hii tunadondoa kwa ufupi mbinu mbalimbali zilizotumika katika utafiti wa makala haya. Miongoni mwa mbinu ni pamoja na mbinu za uchanganuzi wa data zilizotumika, watafitiwa waliohusika katika utafiti huu pamoja na mbinu za ukusanyaji wa data.

3.1 Watafitiwa

Watafitiwa waliohusishwa ni wazazi, walimu pamoja na wanafunzi (kwa maana ya watoto). Wazazi walihitajika ili kutoa mtazamo wao kuhusu malezi, matokeo ya malezi na katika kujenga kesho ya watoto wao. Pia, watafiti walihitaji kujua namna wazazi wanavyotumia lugha katika kutekeleza nafasi yao ya malezi kwa watoto wao. Ama kuhusu walimu, watafiti walikusudia kupata data ya namna walimu wanavyowasiliana na wanafunzi na matokeo ya matumizi mazuri ama mabaya ya lugha kwa wanafunzi wao. Hatimaye, watoto (wanafunzi) walikusudiwa kutoa data ambazo zitaonesha athari ya lugha (mbaya/nzuri) kwao kutoka kwa walimu au wazazi.

3.2 Mbinu za Ukusanyaji wa Data

Utafiti huu ulitumia data zote mbili: za uwandani na za maktabani. Data za uwandani zilikusanywa Mkoa wa Mbeya, Halmashauri ya Jiji la Mbeya. Utafiti ulihusisha wazazi, walimu na wanafunzi (watoto) ili kupata data zenye uwiano. Utafiti ulitumia mbinu ya mahojiano katika vikundi lengwa, dodoso na hojaji pale ambapo muda ulikuwa tatizo hasa kwa walimu. Mbinu ya hojaji ilitumika sana kwa wazazi ili kupata kujua mtazamo wao kwa watoto na maisha yao ya baadaye. Mbinu ya vikundi lengwa ilitumika sana kwa watoto (wanafunzi) ili kuwafanya wawe huru kusema pasi na kuogopa. Fauka ya hayo, utafiti ulikusanya data zake kwa njia ya maktabani ambapo maktaba ya Chuo Kikuu cha Kikatoliki Mbeya ilitumika. Makala, vitabu, magazeti yalisomwa ili kupata data sahihi. Hali kadharika, data pia zilipatikana mkondoni kwa kuperuzi.

3.3 Uchanganuzi wa Data

Data zinaweza kuchanganuliwa kwa kutumia mikabala miwili, ambayo ni mkabala wa kiidadi na mkabala wa maelezo (Kothari, 2014). Mkabala wa kimaelezo au usio wa kiidadi ni mbinu ya kuchunguza data ambayo mtafiti hueleza na kufafanua data zake kwa kutumia maelezo (Masasa, 2017). Kwa hiyo, utafiti huu ulitumia njia hii ya pili ya uchanganuzi wa data zake.

4.0 Uwasilishaji na Uchambuzi

Kama ilivyoelezwa hapo awali, makala haya yamekusudia kujadili matumizi ya lugha katika malezi ya watoto yanavyoathiri ujifunzaji na mustakabali wa maisha yao. Katika makala haya, tumejikita kuwasilisha matumizi ya lugha katika muktadha wa nyumbani, muktadha wa elimu, na muktadha wa kijamii.

4.1 Matumizi ya Lugha Katika Muktadha wa Nyumbani

Nyumbani ndiko msingi wa maisha ya mtoto hujengwa. Ualimu wa nyumbani unatokana na matendo zaidi ya maneno. Mtoto huwa na mzazi/mlezi kila uchao. Hivyo, hutumia muda mwingi kutoa maelekezo ya tabia njema. Aidha, kupitia maneno na lugha inayozungumzwa nyumbani ndiyo humjengea mtoto misingi ya maisha ya baadaye. Mbogo (2010) anasema, mtoto hazaliwi na imani yoyote kuhusu yeye, ubongo wake ni msafi lakini ulio tayari kupokea maarifa ya kila aina, hauna mawaa, lakini mchakato wa malezi, watu wengine, wazazi na marafiki na hata

baadhi ya walimu wanashika kalamu iitwayo ulimi na kuanza kuandika programu tasa ndani ya ubongo na ndani akili changa ya mtoto.

Maelezo hayo ya Mbogo (keshatajwa) yanakuzwa na Safwat na Sheikany (2014) anayesema kuwa, mawasiliano mazuri baina ya wazazi na watoto ni muhimu kwa kuwa huwapatia watoto uwezo zaidi wa kujifunza lugha na kuwandaa kiakili. Mzazi, kama mwalimu wa kwanza, analo jukumu la kuumba tabia na kukuza vipaji kupitia lugha anayotumia wakati wote wa malezi. Ngwiri (2008) anaongezea kuwa, kupitia mazungumzo na matendo ya wazazi, watoto hukuza hali ya kujiamini na kutekeleza mambo kadhaa katika jamii. Lugha wanayotumia wazazi katika malezi huathiri jinsi mtoto anavyokua na kuendelea.

Makuzi na maendeleo bora ya mtoto pia huchangiwa na jitihada za wazazi au walezi kumjenga mtoto kuelekea kufanikisha matamanio yake (Mekacha, 1993 na Ngonyani 1994). Kwa mfano, mzazi au mlezi anapotumia lugha ya ukali huacha majeraha mengi kwa watoto kiakili na kimwili tangu wakiwa wadogo mpaka wanapokuwa watu wazima. Kwa mfano: *'We acha ujinga wako', 'Huyu mtoto walakhi atakuwa mwizi, 'Huyu mtoto hana kipaji cha kuimba, hana!', 'Ee ana sauti kama chura', 'Aa! Huyu ni mbumbumbu mzungu wa reli', 'Nakwambia huyu mtoto atakuwa Malaya kama mamake!', 'We Aisha nimekwambia kwako ni jikoni hizo kazi waachie wanaume', 'We ni mwanamke tu', 'Huwezi, huwezi, huwezi', 'Hufai, hufai, hufai kitu', 'Mbwa wee', na 'Huna akili! Na kadhalika.*

Mzazi akiwa na tabia ya kumwambia mtoto wake kila siku maneno hayo yenye lugha ya kukatisha tamaa, bila kujalisha kuwa alilenga kukaripia, kuonya kama wasemavyo Wanaethnografia kuwa hayo yote ni jukumu la lugha, kuna kitu kingine kinachojengeka zaidi ya hapo kwa huyo anayeambiwa hivyo kila siku. Katika mahojiano na baadhi ya watu, kuna wengine walisema kuwa kuna lugha za kukatisha tamaa walizokuwa wakitamkiwa na watu wao wa karibu zimewaathiri mpaka sasa. Lugha hizo ni kama vile *"We kichaa njoo hapa! Muone akili kama za mamako au babako, lione vile kichwa chake",* na mengine mengi yanayofanana na hayo.

Lugha ya namna hiyo na maneno mengine yanayofanana nayo yamewaathiri sana watu wengi. Katika mahojiano, kuna mtoto alipoulizwa, 'kwa nini hufanyi vizuri darasani'; mtoto akajibu, "*Nimefanana na baba yangu."* Maelezo yanatujulisha kuwa mtoto huyu inawezekana kuwa

huwa anaambiwa kuwa 'huna akili kama baba yako'. Maelezo haya yanashadadiwa na Grice (1989) anaposema vipengele vinavyofaulisha mawasiliano hususani nia ya mwasilishaji, matumizi ya lugha yanayolandana na nia yake, na mikakati inayotumiwa na msimbuaji ujumbe kuelewa kusudi la mwasilishaji ujumbe, huweza kumuathiri mpokea ujumbe.

Changamoto wanazopata watoto wengi katika jamii hutokana na mbinu wanazotumia wazazi wao kuwalea na lugha wanayoitumia wakati wa malezi. Ndiyo maana Gregory na Carroll (1978) wanasisitiza utumizi wa lugha katika muktadha uzingatie uteuzi mzuri wa maneno ili kutoleta athari hasi kama ambazo wazazi wengi wamekuwa wakiwasababishia watoto. Katika utafiti huu tumegundua kuwa maneno mengi yanayotamkwa na wazazi huwa yanamtengeneza mtoto kuwa mtu fulani katika maisha yake. Maneno huwa yanaumba kitu kwenye maisha ya mtu. Mbogo (2010) katika riwaya ya *Siri za maisha* anasema, ubongo ni diski yenye uwezo wa kuhifadhi taarifa zote ama programu zae au programu tasa, ubongo ukisikia maneno hayo kwa muda mrefu huchipua programu kulingana na maneno hayo.

4.2 Matumizi ya Lugha Hasi katika Muktadha wa Elimu

Elimu imekuwa kipaumbele kitaifa kwa serikali. Uchumi wa nchi na maendeleo ya jamii kwa sehemu kubwa hutegemea sana katika uwezeshwaji wa elimu. Eneo la kupatia elimu ni rasilimali inayoweza kutoa ujuzi unaotakiwa ili kupeleka maendeleo mbele. Elimu bora inaweza kuinua familia na jamii kwa ujumla. Kwa bahati maisha yalivyo kwa nyakati hizi, wazazi wengi wanawahi kuwapeleka watoto shuleni. Hivyo, wengi wao huwa bado wana umri mdogo ambao akili yao haina mambo mengi, hunasa kila kitu anachosikia kutoka kwa walimu wake.

Ubongo wa mwanadamu umeumbwa kupokea na kutunza kumbukumbu ya yanayotokea. Wataalamu mbalimbali wanasema mtoto ana uwezo mkubwa sana wa kupokea taarifa na kutunza kumbukumbu zaidi ya mtu mzima. Hii inasababishwa na mtoto kufikiri wakati uliopo tu tofauti na mtu mzima. Kwa hiyo, hayo anayoyatunza akilini humsaidia kuchanganua na kutoa maamuzi mbalimbali katika maisha ya kila siku. Matendo na misemo huunda taswira vichwani mwa watoto juu ya maisha, lugha na mahusiano. Kwa mfano, Mbogo (2010:25) ametoa mfano huu kuhusu mwalimu anavyoweza kuharibu mustakabali wa maisha ya mtoto ikiwa anatumia lugha hasi kama ifuatavyo:

We Joni, huna akili

We Joni mbumbumbu, kaa kando

We Joni uzembe umekusharabu mwilini

We Joni kila kitu ni wa mwisho

Katika mfano huo hapo juu, matokeo yake mtoto Joni ataamini na atakubali kuwa maisha yake yote yeye ni mjinga, hana akili, hii ina maana wakati wowote fursa ikitokea ya kujipatia maendeleo, ustawi ama mafanikio maishani John hatakuwa na imani wala jusura ya kujaribu.

Mwanasaikolojia Skinner (1957) anasema kuwa, mazingira mazuri ya ujifunzaji wa mwanafunzi huchangia uelewa mzuri wa mwanafunzi. Mtoto anapokosea arekebishwe na siyo akatishwe tamaa na asifiwe pale anapofanya vizuri. Kwa isivyo bahati sana, baadhi ya walimu hutumia lugha chafu, zenye ukatili na wakati mwingine zenye kukatisha tamaa. Ni mara chache hutoa lugha za kuwatia moyo wanafunzi hasa wale wenye uwezo mdogo. Wanaethnografia wanasema kuwa, maudhui ya lugha ni nguzo muhimu katika kuteua maneno muafaka katika mawasiliano. Hivyo basi, ni muhimu na ni vizuri walimu wakawa makini sana na lugha wanayotumia wakati wa ufundishaji, kwa sababu ufundishaji ni sehemu ya malezi. Katika utafiti huu tumebaini kuwa kuna athari azipatazo mwanafunzi katika muktadha wa elimu zinazochangia kuharibu ama kujenga mustakabali wa maisha ya mtoto/mwanafunzi.

4.2.1 Athari ya matamshi kwa mtoto

Katika kipengele hiki tunakusudia kuonesha athari ya utumizi wa lugha, athari yaweza kuwa chanya au hasi. Kwa hiyo, katika makala haya, tutajikita kuelezea athari hasi ambazo kwazo tunaona ni ukatili, ambao mtoto anafanyiwa kwa kujua au bila kujua. Tunaona ni ukatili kwa sababu athari ya mtoto kutamkiwa lugha mbaya/chafu katika maisha yake ni sawa na kumfanyia mtoto huyo ujahili, ubedui, au udhalimu. Athari hii ya utumizi wa lugha ya ukatili tunaiangazia katika kipindi ambacho mtoto anakuwa katika mazingira ya shule, hivi kuwa chini ya ulezi wa walimu. Tunachunguza namna walimu wanavyowajibu na kuzungumza na wanafunzi, adhabu zinazoambatana na lugha pamoja na usahihishaji wa kazi za wanafunzi. Kwa hiyo, makala haya yamebainisha aina za athari lugha wanazopata wanafunzi katika ngazi mbalimbali za elimu. Athari dhidi ya wanafunzi hujitokeza kwa namna tofauti tofauti. Inaweza ikawa kimwili,

kisaikolojia, au kifikra. Katika utafiti huu tumegundua kuna lugha za kikatili zinazotumiwa na baadhi ya walimu katika muktadha wa elimu. Aina za athari zilizojadiliwa katika makala haya ni zile zinazosababishwa na ukatili lugha: ukatili lugha wa kisaikolojia, ukatili lugha wa kimatendo, ukatili lugha wa kifikra kama vile ishara za maandishi, na matamshi ambayo hubainika katika vitisho vya matamshi, na pia ukatili wa kuzisoma kazi za wanafunzi zenye kuambatana na maandishi ya kuvunja moyo.

Kwa jumla, ukatili lugha huu unaweza ukafanyika mbele za watu, faraghani au mtandaoni. Bila kujali unafanyika vipi, wapi na umetekelezwa na nani au ni kwa sababu gani, ukatili wa lugha katika elimu una madhara makubwa ya muda mfupi na muda mrefu na huzuia ushiriki kamilifu katika jamii zao. Watafitiwa wengi waliohojiwa katika ngazi mbalimbali walidhihirisha haya. Kwa mfano, watafitiwa kumi walihojiwa kati ya watafitiwa thelathini walisema kuwa waliacha shule na sasa wanaishi maisha waliyonayo kwa sababu walimu wao waliwaathiri kwa lugha waliyotumia hata wakaamua kuchagua mkondo mwingine wa maisha mbali na shule. Kwa mujibu wa Crystal (1977), kinachovutia katika kuibua maana katika sanaa ni muktadha wa maongezi. Muktadha huchukua wajibu mkuu katika kubainisha jinsi maneno mahsusi yanavyobainishwa katika tukio hilo.

4.2.1.1 Athari za ukatili lugha wa kisaikolojia

Wanaethnografia ya Mawasiliano wanadadavua kuwa lugha shurti izingatie mandhari na wahusika. Zaidi pia, ujumbe unaowasilishwa huwa nguzo muhimu katika kuteua maneno mwafaka katika mawasiliano. Ukatili wa kisaikolojia ni pale mtu anapotendewa matendo yanayomsababishia maumivu ya kiakili na/au kihisia ambapo mtu mwingine hawezi kutambua kuwa mwenzake ametendewa ukatili hadi mazingira yatakapojitokeza na mtendewa akajieleza. Mfano wa ukatili huu ni matusi kwa njia ya maneno au ishara yenye lengo la kudhalilisha, vitisho na kutishia kufanya fujo, maneno ya kufedhehesha, kudharauliwa hadharani, kutishia, kutoa siri, kuingiliwa faragha, kutishiwa, na kadhalika. Wanafunzi wanaathiriwa na matendo ya kikatili na lugha za kikatili zinazotumiwa na walimu wao. Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa kuna lugha ngumu ambazo wanafunzi hutamkiwa na walimu wao kama vile, "*Kenge na nusu, watoto wa farao, mbuzi wa kafara, ndama, wajinga,"* na kadhalika.

Katika kutafiti kipengele cha matumizi ya lugha kuwa ni kwa namna gani lugha inaleta athari nzuri au mbaya katika maisha ya mtu, imeonekana kuwa kuna athari kubwa mwalimu anapomjibu mwanafunzi kwa lugha isiyo nzuri mbele ya wanafunzi wenzake au hata akiwa pekee. Kwa mfano, walimu wamekuwa na kaida ama kasumba ya kuuliza maswali ya papo kwa papo wawapo darasani. Licha ya walimu wengi kutopenda kuulizwa maswali na wanafunzi, walimu wengi huwa wana tabia ya kusema jambo kumhusu mwanafunzi aliyejibu. Hapa tutarejelea mfano wa makala iliyochapwa kwenye gazeti la *Mwananchi* (2017, Machi 19) inayoitwa 'Maneno ambayo Wazazi Hawapaswi Kuyatumia katika Kuwaasa Watoto'. Mwandishi anatoa mfano wa mwalimu aliyeuliza swali kwa wanafunzi wake, mwanafunzi wa kwanza hakutoa jibu sahihi. Mwanafunzi wa pili akajibu kwa usahihi. Kupata au kukosa ni sehemu ya ujifunzaji lakini mwalimu alitumia lugha ambayo ni hasi kwa wanafunzi wote wawili. Tumedondoa mfano huo hapa chini.

> *"Nilijua kuwa huyu mpumbavu asingeweza kupata jibu sahihi"*
> *"Leo mvua itanyesha. Huyu mpumbavu amepata jibu sahihi!" (Akacheka sana)*
> (*Mwananchi*, 19/03/ 2017)

Fikiria ungalikuwa wewe ndiye mwanafunzi wa kwanza ambaye umefikiria jibu, umetumia nguvu kufikiri, hukukataa hata ulipoambiwa ujibu na ukajaribu kwa moyo, halafu, mwalimu anahitimisha kwa kukunenea maneno yaliyo katika (a). Ungalijisikiaje? Ungalijionaje mbele ya wanafunzi wenzako? Ungalikuwa na nguvu tena ya kujaribu, kujifunza ama kuwa na moyo wa kuwa makini katika vipindi vya mwalimu huyo?

Fikiria tena mwanafunzi wa pili ambaye alijibu swali husika na akapata. Badala ya mwalimu kumtia moyo anacheka, hata wanafunzi wenzake wanaungana na mwalimu kucheka. Hatimaye mwalimu anaona kupata kule kwa mwanafunzi ni sawa na maajabu ya dunia. Unaweza kufikiria namna gani mwanafunzi huyo alivyojisikia baada ya kuambiwa hivyo na mwalimu wake?

Inawezekana mwalimu aliongea kauli hizo kwa kujifurahisha mwenyewe. Inawezekana mwalimu huyo alitoa kauli hizo akidhani ni utani ambao unafurahisha darasa, kwa hakika hapa tukimfikiria mwalimu tutabaki kusema 'inawezekena… inawezekana…' na hatutofika hitimisho. Hata hivyo, tunaweza kutumia mfano huu kueleza kuwa lugha ina kazi zaidi ya kuwezesha

mawasiliano. Mathalani, kwa mwanafunzi wa kwanza, inaonekana mwanafunzi huyo huambiwa mara kwa mara na mwalimu kuwa hana akili. Ndiyo maana hata alipokosa mwalimu karejelea kauli yake. Maneno haya ya mwalimu yanaua kujiamini kwa mwanafunzi. Yanapojirudia kichwani mwa mwanafunzi yanamfanya aamini kuwa hana akili. Haya yote yanahitimishwa na mwanafunzi kuamini kuwa atafeli katika mtihani wa mwisho na hivi kuua kabisa ndoto zake alizopata kujiwekea. Hata mwanafunzi aliyepata swali bado hakustahili maneno yale aliyoambiwa na mwalimu. Hii inatufanya tusisitize sana kwa walezi (walimu) kuwa makini waongeapo na wanafunzi kwani maneno huumba na kujijenga ndani ya kichwa cha mwanafunzi.

Ukatili huu wa maneno ya lugha unaleta athari hasi kwa watoto. Katika makala hiyo iliyochapwa kwenye gazeti la *Mwananchi* (limekwishatajwa), mwandishi anatoa mfano wa mama aliyekuwa akikaripia alipoona mtoto wake mmoja anamnong'oneza jambo wakati wakila chakula. Mama akakaripia kwa kusema "*Wewe mjinga funga kopo lako na endelea kula."* Tunafahamu kuwa kuna wazazi wenye maneno ya kukera zaidi ya haya, ambayo huwaambia watoto wao kila siku. Ukijaribu kufikiria athari ya maneno katika akili na maisha ya mtoto/mwanafunzi huyu utabaini kuwa ni mbaya sana. Kwa mfano, fikiria kama mtoto huyu ndiye yule aliyetukanwa na mwalimu kuwa ni '*mpumbavu'* na kwamba hana uwezo darasani ndiyo maana hawezi kupata swali. Chukulia kwamba mtoto huyo ni wa darasa la kwanza. Inatarajiwa ya kuwa ataendelea kuwa na mwalimu huyo kwa miaka zaidi ya mitano. Na huku nyumbani mama yake ataendelea kuwa naye hadi awe mtu mzima au majaaliwa ya Mola. Ni wazi kuwa mtoto huyo atakuwa 'kiumbe wa ajabu' sana katika jamii yake.

4.2.1.2 Athari ya ukatili lugha wa kimatendo

Ukatili lugha wa kimatendo ni ule unaotokana na utoaji adhabu unaoambata na matamshi au maneno mabaya kwa mwanafunzi/mtoto. Adhabu, kwa kawaida, hutolewa kwa mtu aliyefanya kosa. Katika mazingira ya shule, kuna adhabu ya fimbo/viboko, adhabu ya kufanya kazi ngumu, japo kutaja kwa uchache. Wakati mwingine wanafunzi wanapokosea, walimu huamua kuwapa onyo kwa karipio kali. Pamoja na dhamira nzuri ya adhabu kwa maana ya kumsaidia mtoto awe na maadili mazuri, baadhi ya walimu hutoa adhabu hizo huku wakisindikiza kwa maneno makali. Kwa mfano:

Mwone akili kama za mama yako

Elimu siyo kwa ajili ya kila mtu…wewe shule haikutaki
Mnatusumbua tu hapa shuleni si mkalime, mkapige debe, n.k.

Ni walimu wachache sana wanaoweza kutoa adhabu kwa wanafunzi pasi na kutoa kauli chafu. Pengine, hali hiyo huchangiwa na kauli ya wahenga kuwa 'ukitaka kumuua mbwa mpe jina baya'. Mwanafunzi hujikuta akipewa adhabu husika (kama ni fimbo au kazi ngumu) pamoja na kuathiriwa kisaikolojia. Anaanza kujiuliza inawezekana mama/baba hana akili ndiyo maana hakufika chuo kikuu au hata kuwa na kazi nzuri. Inawezekana sisi (familia yetu) tuliumbwa tusisome ndiyo maana si kaka wala dada zangu aliyefika mbali kitaaluma. Kwa hiyo, mwalimu anakuwa chanzo cha kuzima ndoto za mwanafunzi. Hii ina athari kubwa kwani mwanafunzi huyakumbuka maneno hayo kila anapotumikia adhabu husika. Maumivu yake humfanya akate tamaa ya shule na ndiyo sababu baadhi ya wanafunzi hujikuta wakiacha shule au kutoroka.

Walimu wengi hutenda ukatili huu karibia kila siku, ama kwa kujua au kutojua. Wanaethnografia wanasisitiza sana (katika mihimili ya mazingira, mada na wahusika) kuwa mzungumzaji (mwalimu) anapaswa kutumia lugha kwa umakini sana (Gregory na Carroll, 1977). Unakuta mwalimu kila anapomchapa mwanafunzi lazima aambatanishe na maneno 'mbwa, huna akili, kichwa maji' na mengine yanayofanana na hayo. Huu ni ukatili mkubwa sana ambao mtoto anakumbana nao. Inapotokea mtu anayemwamini anamwambia (kila siku) hana akili, na akijichunguza hata maendeleo yake kitaaluma ni mabaya walimu husema hivyo, huamua kukata tamaa. Makala haya yanasisitiza jamii kuwa makini na maneno wayasemayo mbele ya watoto/wanafunzi.Uteuzi wa maneno mwafaka katika mawasiliano ni nguzo muhimu sana katika ujengaji wa akili ya mtu, hivyo ni vyema sana kuchagua lugha nzuri itakayomfanya mtoto ajione kuwa naye ni sehemu ya jamii na analofanya linathaminiwa.

4.2.1.3 Athari ya ukatili lugha wa kifikra

Athari ya kuwa na mtazamo hasi katika jambo fulani kutokana na kauli alizowahi kuambiwa. Wakati wa usaili, tuliwahoji wanafunzi walioonekana kufeli kozi ya Fonolojia inayofundishwa kama somo Chuo Kikuu. Swali hili lilijibiwa na wanafunzi kwa majibu tofautitofauti. Wanafunzi wa somo hilo walionesha kuwa na mtazamo hasi na somo husika. Kwa mfano, *"Kwa kweli hili somo mimi ni gumu kwa sababu hata mwalimu wetu wa kidato cha tano na sita alishatuambia*

na yeye alisema alifeli akiwa chuo." Kauli nyingine zilizotolewa na wanafunzi hao (waliohojiwa) ni pamoja na zifuatazo:

> Mimi nilishaambiwa na mwalimu wangu siwezi Fonolojia nikiwa sekondari, kwa hiyo siipendi. Ndiyo maana sishangai kuwa nimefeli.
>
> Nimefeli kwa sababu mwalimu alisema Fonolojia si ya kila mtu! Ni watu wachache tu wanaweza kuisoma.

Ukichunguza na kufikiri kauli hizi za wanafunzi pasi na shaka utapata kubaini mambo kadha wa kadha kichwani mwako mathalani wanafunzi hawa si kweli kwamba hawana akili. Kwa sababu kama wasingekuwa na akili wasingeweza kufika Chuo Kikuu. Wanafunzi hawa walishafeli kozi hiyo tokea siku ya kwanza wanaanza kuisoma kwa sababu akili yao haikuwa tayari kupokea maelezo mengine, ilhali watu waliowaamini walishawadhihirishia kuwa hawawezi. Ndiyo maana tunasisitiza katika makala haya kuwa pamoja na kazi nzuri ya lugha kuwezesha mawasilino pia inamjenga mtu bora au kumharibu mtu huyo. Baada ya kubaini haya, tuliamua kuwahoji wanafunzi wa masomo ya sanaa sababu za wao kutokwenda kusoma masomo ya sayansi na hesabu. Miongoni mwa majibu yao yalikuwa kama ifuatavyo:

> Sikwenda huko kwa sababu baba yangu alishaniambia sayansi ni ngumu.
>
> Kaka na dada yangu wote walinionya mapema kuwa kama nataka nifaulu nisichukue sayansi au hesabu
>
> Tulipokuwa kidato cha tatu mwalimu alinikatalia nisiingie kwenye vipindi vya sayansi … eti sina akili.
>
> Tuliambiwa tukiwa sekondari kuwa sayansi si ya kila mtu.

Wanafunzi hawa ni wazi kuwa (inawezekana) watakuja kuwaambia watoto wao, wadogo zao na hata marafiki zao vivyo hivyo. Hii ni kwa sababu waliambiwa na wakaamini na sasa ndiyo mitazamo yao. Data hii pia inatuonesha athari ya kauli za wazazi ama walimu katika kuyachukulia masomo. Kwa hakika walimu na wazazi wanapaswa kuwa waangalifu kwa kauli zao kwani hawana nafasi ya kuzifuta vichwani mwa wanafunzi. Huu ni ukatili kama ukatili mwingine ambao unamwathiri mtu kisaikolojia.

Walimu wengi, mara nyingi, hupenda kutoa maoni kwa kuandika maneno mazuri kwa mwanafunzi anayeonekana kufaulu mtihani pindi wanaposahihisha. Hali kadhalika, walimu hao hawaachi kumwandikia maneno ya kukera au kumchorea kielelezo cha kukera mwanafunzi anayeonekana kufeli somo husika. Murimi (2017) anadadavua kuwa katika usahihishaji wowote, utuzaji hutolewa kama namna ya kuonesha uamuzi wa mwalimu kuhusiana na kazi ya mwanafunzi. Na uamuzi huu ndiyo humpa nafasi mwalimu kutumia maneno kama, 'vema, vizuri, kazana, safi sana, n.k, kwa upande mmoja. Pia, humpa fursa hiyohiyo mwalimu kumwandikia mwanafunzi aliyefeli 'ongeza bidii, mbaya sana, ovyoo, achana na hili somo, au kumchorea bichwa likitoa machozi, kwa upande mwingine. Ama kwa hakika, maoni haya hutolewa kuhusiana na udhaifu au ubora wa kazi ya mwanafunzi (Richard, 1971).

Katika kuzungumzia suala hili la kutoa maoni kwa mwanafunzi hasa baada ya kusahihisha kazi ya mwanafunzi, James (1999) anadai kuna aina ya kwanza ya utoaji maoni haya ambayo ni ya matamshi ya moja kwa moja kutoka kwa mwalimu hadi kwa mwanafunzi. Anaeleza zaidi kuwa maoni ya namna hii hutolewa ofisini ambapo mwalimu huwa na mwanafunzi. Aina hii, licha ya kuwa na makusudio mazuri, baadhi ya walimu hutumia lugha ya ukali, vitisho au karipio ambalo humfanya mwanafunzi ajisikie vibaya na pengine kukata tamaa kabisa. Ndiyo maana Wanaethnografia wanasisitiza sana suala la matumizi ya lugha kwa kuzingatia mazingira pamoja na wahusika ambapo kwa hapa ni mwalimu na mwanafunzi . Aina nyingine iliyotajwa na James (keshatajwa) ni ile inayohusu utoaji wa maoni andishi pembeni, juu au mwishoni mwa insha/kazi ya mwanafunzi. Maoni haya pia ndiyo tuliyopata kudokeza hapo juu kuwa yakiandikwa vibaya hukera, huchefua na hukatisha tamaa wanafunzi.

Mwanafunzi mmoja wa shahada ya awali (mwaka wa kwanza) anayesoma Shahada ya Sanaa na Ualimu, akisoma somo la Kiswahili na Kiingereza, alipoulizwa kwa nini hakutaka kusoma somo la hesabu alisema:

> *Nilipokuwa kidato cha kwanza, tulifanya jaribio. Mimi nilifeli na mwalimu alinichorea 'buyu' linalolia. Nikavumilia. Mara ya pili nilifeli, sikupata sifuri, ila mwalimu akaniandikia kuwa halikuwa somo langu. Akimaanisha, Hisabati ni somo la watu wachache wenye uwezo. Kuanzia hapo nilianza kulichukia na hata kwenye vipindi vyake nikawa siingii* (Usaili kwa Mwanafunzi wa Mwaka wa Kwanza: 2025).

Maelezo ya mwanafunzi huyu yanaonesha kuwa utumizi wa lugha ya mwalimu katika kutoa maoni yake ulikuwa na athari kubwa kwa mwanafunzi. Suala la kutoa maoni katika kazi ya mwanafunzi ni zuri na linaungwa mkono na wataalamu kama Vengadasmy (2002) na Roberts na wenzake (1989) kama walivyonukuliwa Murimi (keshatajwa). Katika kutilia mkazo matumizi la lugha ya utoaji maoni katika kazi za wanafunzi, Murimi (2017) anahitimisha kwa kudai kuwa maoni yaliyotolewa vyema kama inavyostahili ni kiungo muhimu sana katika kuboresha ubunifu na uandishi wa kazi ya mwanafunzi. Lakini, maoni haya yakitolewa visivyo huwa na athari kubwa sana katika maisha ya mtoto/mwanafunzi.Katika suala la uteuzi wa maneno wanaethnografia wanasisitiza kuwa, tunapaswa kuchagua maneno kulingana na wahusika na mazingira, yaani unatakiwa uongee nini, kwa nani na katika mazingira gani.

4.3 Matumizi ya Lugha katika Muktadha wa Kijamii

Jamii ni mkusanyiko wa watu wanaoishi kwa pamoja katika eneo moja la kijiografia wakiunganishwa na historia yao na wakitambuliwa kwa utamaduni wao; lugha, mila na desturi. Tunahitaji lugha katika maisha yetu ya kila siku. Tunapofikiri mambo yaliyopita, yaliyopo na yajayo tunatumia lugha. Tunapowasiliana na wengine, tunahitaji lugha. Katika muktadha huu, lugha ni nyenzo muhimu inayotuunganisha na watu wanaotuzunguka. Matumzi ya lugha ni katika miktadha mbalimbali ya mazungumzo. Matumizi ya lugha ni dhana pana kwa maana kwamba imebeba mawasiliano ya wanajamii. Mawasiliano hayo yanaweza kuwa katika muktadha wa mazungumzo au maandishi (Msanjila na wenzake, 2011). Kwa mujibu wa King`ei (2010), katika muktadha wa mazungumzo, wazungumzaji hushawishika kutumia aina fulani ya lugha ambayo hutofautiana na muktadha mwingine. Hoja hii inachukuana sana na hoja za Wanaethnografia kama vile Gregory na Carroll (1977) na Crystal (keshatajwa) ambao kwa pamoja wanasisitiza kuwa matumizi ya lugha shurti yazingatie muktadha pamoja na wahusika. Makala haya yanatoa wito kwa wanajamii kwa ujumla kutumia lugha nzuri kwa watoto, bila kujali mtoto huyo ni wa nani. Inapotakikana mtoto kukaripiwa basi akaripiwe kwa kutumia lugha yenye staha na kwa kuzingatia umri/rika la mtoto. Hii itaifanya jamii kuitengeneza dunia kuwa sehemu nzuri na salama kwa kuishi watu wa rika zote.

5. Hitimisho

Zombwe (2008) anasema kuwa mafanikio ya mtu mzima huchangiwa na malezi ya utotoni pamoja na mwingiliano wa mazingira na jamii yake. Wazazi au walezi wakifanya jitihada

kumjenga mtoto na kumuandaa mtoto kuwa raia makini anayejitambua, mchango wa mtoto huyo kwa maendeleo ya jamii utakuwa mkubwa na familia yake itanufaika zaidi. Makuzi na maendeleo ya mtoto yanachangiwa na wazazi, familia, na jamii kwa jumla. Hivyo basi, ni muhimu wazazi na walezi kuwatunza na kuwalea watoto kwa kufuata misingi inayotakiwa. Kwa kuzingantia Nadharia ya Ethnografia ya mawasiliano, utafiti huu umebainisha umuhimu wa muktadha, hadhira na utamaduni katika kuainisha lugha na matumizi yake katika malezi. Nadharia hii ilitumiwa katika kufafanua jinsi ambavyo maneno katika muktadha wa malezi yanavyoweza kusababisha aidha madhara au mambo mazuri.

Marejeleo

BAKITA (2022). *Kamusi Kuu ya Kiswahili*. Long Horn.

Crystal, D. (1977). *English as a global language*. Cambridge University Press.

Fasold, R. (1990). The sociolinguistics of language in *Introduction to Sociolinguistics*, 2. Basil Blackwell.

Gregory, M. & Carroll, S. (1978). *Language and situation: Languages varieties and their social context.* Routledge and Kegan Paul.

Grice, H. P. (1989). *Studies in the way of words*. Harvads University Press.

Gregory, G. & Carroll, S. (1978). Language and situation: *Language Varieties and their Social Contexts*. Routledge.

Goodman, R (2005). *Pragmatism, critical concepts in philosophy*. Routledge.

Horn, L. (1990). *Pragmatic theory*. Cambridge University Press.

Hymes, D. (1962). *Ethnography of speaking, anthropology and human beahaviour*. Cambridge University Press.

Hymes, D. (1964). *Language in culture and society*. Harpernand Rowa Inc.

Hymes, D. (1972). *Foundations in social linguistics: An ethnographic approach*. University of Peensylavani Press.

Hymes, D. H. (1974). Ways of speaking. In R. Bauman & J. Sherzer (Eds.), *Explorations in the ethnography of speaking* (pages 433–452). Cambridge University Press.

Hymes, D. (1974). *Foundations in sociolinguistics: An ethnographic approach*. University of Pennsylvania Press.

Hudson, R. A. (1980). Languages. In *Sociolinguistics*. Cambridge: CUP.

King'ei, K. (2010). *Misingi ya isimu jamii*. TUKI.

Kobia, M. (2008). *Taswira za kiuana katika nyimbo za tohara za wanaume miongoni mwa jamii ya wigembe*. Tasnifu ya Uzamivu ya Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Kothari, R. C. (2014). *Research methodology, methods and techniques* (3rd ed.). New age International (P) Ltd.

Kyeu, D. (2021). *Nadharia ya ethinografia ya mawasiliano*. Chuo Kikuu cha Calfonia, Marekani. Imepakuliwa tarehe 15/03/2025 saa 06:20 mchana kutoka https://www.academia.edu/49063967/NADHARIA_YA_ETHINOGRAFIA_YA_MAWASILIANO_Dkt_Kyeu

Leech, G. (1969). *A linguistic guide to English poetry*. Longman.

Mwananchi (March 19, 2017). Maneno ambayo wazazi hawapaswi kuyatumia katika kuwaasa watoto. Imepakuliwa kutoka https://www.mwananchi.co.tz/mw/habari/makala/johari/maneno-ambayo-wazazi-hawapaswi-kuyatumia-katika-kuwaasa-watoto-2841820

Massamba, D. P. B. (2009). *Kamusi ya falsafa ya lugha*. TUKI.

Masasa, J. I. (2017). Kuchunguza athari ya matamshi ya lugha ya kijita katika kujifunza lugha ya Kiswahili. Chuo Kikuu Huria. Imepakuliwa 15/03/2025 saa 7:00 mchana kutoka https://www.google.com/url?sa=t&source=web&rct=j&opi=89978449&url=https://repository.out.ac.tz/2445/1/JOSEPH%2520ISMAIL%2520MASASA%2520TASNIFU%2520YA%2520UTAFITI.pdf&ved=2ahUKEwjmzLyi5YuMAxV1SvEDHfbhGXsQFnoECAkQAQ&usg=AOvVaw1ZZLLtoQ3uEuUgRpUadMQN

Mekacha, R.D.K. (1993). The sociolinguistic impact of Kiswahili on ethnic community languages in Tanzania: a case study of Ekinata. *African studies series, rican studies series*. Bayreuth: Bayreuth Univ. xiv+237pp dissertation.

Mbogo, E. (2010). *Siri za maisha*. E$ D Vision Publishing Ltd.

Mochiwa, Z. (2007). Utoto hadi ungumbaru: Matatizo ya Kiswahili katika elimu. Dar es Salaam. TUKI.

Murimi, J. N. (2017). Maoni andishi katika usahihishaji wa insha za wanafunzi katika *IJRDO-Journal of Educational Research.* 2, Sept 2017.

Ngonyani, D. S. (1994). *A classification of southern Tanzanian languages*. University of California at Los Angeles MA thesis. (viii+52pp.)

Ngwiri, L.N. (2008). *Powerful parenting: What every parent should know*. Printpac.

Richards, J. C. (1971). Error analysis and second language strategies. *Language Science*, 17, 12-22.

Robert, P., Judith, A. na John, F. (1989). *The effective teaching of English*. Audison Wesley Longman Ltd.

Safwat, R. F., na Sheikany, A. R. (2014) *Effect of parent interaction on language development in children*. https://doi.org/10.4103/1012-5574.138488

Skinner, B. F. (1957). *Verbal behavior.* Appleton-Century-Crofts. https://doi.org/10.1037/11256-000

Verial, D. (2018). *The effects of environment on a child's behaviour*. Retrieved from https://www.hellomotherhood.com/the-effects-of-environment-on-a-childs-behavior-4892177.html.

Zombwe, G. M. (2008). *Civics for secondary schools: Book two*. Nyambari Nyangwine Publishers.